# BWANA AMEJAA HURUMA NA NEEMA - II

***Alex Rwelamira***
***29.08.2026***
***DSM***




**1. Ee nafsi yangu umhimidi Bwana, naam, vyote vilivyo ndani yangu,**
**Vilihimidi jina lake takatifu/**
**Ee nafsi yangu umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili zake zote.**

**2. Ndiye anayekusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote/**
**Aukomboa uhai wako na kaburi, akutia taji la fadhili na rehema.**

**3. Yeye hatateta siku zote, wala hatashika hasira yake milele/**
**Hatutendei kadiri ya hatia zetu, wala halipi kwa kadiri ya maovu yetu.**

**4. Maana vile mbingu zilivyoinuka juu ya nchi,**
**Kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao/**
**Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi,**
**Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.**